

HALMASHAURI YA WILAYA YA MASWA

SHULE YA SEKONDARI JIJA,
S.L.P. 59,
MASWA – SIMIYU.
SIMU 0759 62 22 63

05/12/2020

Kumb Na. JSS/279/JI/VOL. I/10

JINA LA MWANAFUNZI SHULE
S.L.P. , MASWA

YAH:- MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI JIJA WILAYA YA MASWA MKOA WA SIMIYU MWAKA 2017.

Ninafurahi kukuarifu kwamba umechaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza (I) katika Shule hii mwaka Shule ya Sekondari Jija iko katika Kijiji cha Jija Kata ya Jija.

Muhula wa kuanza masomo unaanza tarehe 11/01/2021 unatakiwa kuripoti shuleni kuanzia tarehe 11/01/2021 na mwisho wa kuripoti ni tarehe

Mambo muhimu ya kuzingatia.

SARE YA SHULE

(a) WASICHANA

- (i) Sketi mbili (2) rangi ya Light blue kitambaa cha suti, ndefu ifunike magoti, inchi 6 chini ya magoti, mkanda wake usizidi nchi mbili (zidakaguliwa shuleni)
- (ii) Shati mbili (2) Tetroni za mikono mifupi, zisishonwe za kubana mwili na ziwe ndefu za kuchomekea wakati wote
- (iii) Tai ndefu rangi ya Light Blue
- (iv) Viatu vyeusi vya ngozi vya kufunika miguu vya kufunga na kamba visivyo na urembo wala visigino virefu, (viatu vyenye urembo ni marufuku shuleni)
- (v) Soksi nyeupe ndefu jozi mbili (stocking)
- (vi) Sweta lenye rangi ya Blue.
- (vii) Rangi ya Hijab kwa Waislamu ifanane na sare ya shule.

THE HEADMASTER
JIJA SECONDARY SCHOOL
S.L.P. 59,
MASWA.



(b) WAVULANA

- (i) Suruali mbili, rangi ya Light Blue, kushona upana na inchi kumi na saba (17) miguuni, mifuko miwili pembeni na mmoja nyuma, ziwe na malinda yasiyozidi matatu na kupungua mawili. (Zitakaguliwa shuleni).
- (ii) Mashati mawili meupe (Tetroni) mikono mifupi.
- (iii) Tai ndefu rangi ya Light blue.
- (iv) Viatu vyeusi vya ngozi vya kufunika vya kufunga na kamba jozi mbili zisiwe na visigino virefu, (Viatu vyenye urembo ni marufuku shuleni).
- (v) Soksi nyeusi ndefu jozi mbili.
- (vi) Sweta rangi ya blue.

(c) Daftari 15, kalamu na mkebe wa Hesabu.

(d) Kamusi ya kingereza kwa kingereza ni lazima aje nayo

1.0 Sheria na kanuni muhimu za shule hii.

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyorekebishwa kwa sharia Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi, yenye dhamana ya elimu nchini na Ofisi ya Waziri Mkuu – TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji Elimu. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yatafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripori shuleni.

- (a) Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii
 - kwa ujumla ni jambo la lazima.
- (b) Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule ni lazima.
- (c) Kushitiki kwa makini kufanya maandalio ya jioni (preparation).
- (d) Kuwahi katika kila shughuli za shule na nyingine utakazopewa.
- (e) Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii.
- (f) Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule.
- (g) Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa.
- (h) Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote na
- (i) Kutunza mali za Umma.

2.0 Makosa yafuatayo yanaweza kusabisha kufukuzwa au kusimamishwa shule.

- (a) Wizi
- (b) Uasherati na ushoga
- (c) Ubakaji
- (d) Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya kama vile uvutaji bangi, cocaine, mirungi, kubeli na kadhalika.
- (e) Kupigana au kupiga
- (f) Kuharibu kwa makusudi mali ya Umma.
- (g) Kudharau bendera ya Taifa.
- (h) Kuwa mjamzito/ kupata mimba
- (i) Kutoa mimba.
- (j) Kugoma, kuchochea na kuongoza au kushiriki kuvuruga amani na usalama wa shule au watu.
- (k) Kukataa adhabu kwa makusudi
- (l) Kuwa na simu ya mkononi

3.0 Siku ya kuripoti mwanafunzi aje shuleni na mzazi au mlezi.

4.0 Tafadhali soma kwa makini maelezo / maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.

KARIBUNI SANA KATIKA SHULE YA SEKONDARI JIJA



.....
GOMBANIA M. CHACHA
MKUU WA SHULE.

